TANGAZO LA SERIKALI Na. 23 la tarehe 12/1/2024

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI,
(SURA. 413)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu 45 (2) (i))*

KANUNI ZA TIKETI MTANDAO ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA, 2024

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MAOMBI NA USAJILI WA MFUMO WA TIKETI MTANDAO

4. Maombi ya kibali cha mfumo wa tiketi mtandao.
5. Vigezo vya utoaji kibali kwa mfumo wa tiketi mtandao.
6. Kuunganisha na uangalizi wa ulinzi wa mitandao.
7. Maamuzi ya maombi.
8. Cheti cha kibali.
9. Kuhuisha cheti cha kibali
10. Kusimamisha au kufuta cheti cha kibali

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA WAENDESHA MFUMO WA TIKETI MTANDAO

11. Mfumo wa tiketi mtandao.
12. Masharti kwa mtoa huduma.
13. Uteuzi wa wakala.
14. Masharti kwa wakala wa huduma ya tiketi mtandao.

SEHEMU YA
NNE
LUGHA YA MFUMO WA TIKETI MTANDAO NA MAUDHUI YA TIKETI MTANDAO

15. Lugha ya tiketi mtandao.
16. Maudhui ya tiketi mtandao.

SEHEMU YA TANO
USIMAMIZI WA MFUMO WA TIKETI MTANDAO

17. Kamati ya Watalaamu wa Mfumo Tiketi Mtandao.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA JUMLA

18. Takwa la mkataba.
19. Uhamisho wa abiria.
20. Makosa na adhabu.
21. Mapitio.
22. Rufaa.

JEDWALI

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI,
(SURA. 413)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu 45 (2) (i))*

KANUNI ZA TIKETI MTANDAO ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA, 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Matumizi ya Tiketi Mtandao, 2024.

Matumizi

**2**. Kanuni hizi zitatumika kwa wamiliki wa mfumo wa tiketi mtandao, watumiaji wa mfumo wa tiketi mtandao ambao wanatoa au kutumia huduma za tiketi mtandao zinazotumika katika huduma zinazodhibitiwa.

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo-

Sura ya 413

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

"wakala" maana yake ni wakala wa mtoa huduma aliyesajiliwa kama mwezeshaji chini ya kanuni zilizotengenezwa chini ya Sheria;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

"tiketi mtandao" maana yake ni tiketi au stakabadhi zinazotolewa kwa abiria kupitia mfumo wa tiketi mtandao ambayo inaweza kuwa kwa njia ya ujumbe wa kielektroniki au nakala iliyochapishwa wakati wa kufanya miamala kwenye huduma zinazodhibitiwa;

"kifaa cha kutolea tiketi mtandao" maana yake ni mashine iliyoundwa kwa ajili ya kutoa tiketi za kielectroniki kwa

watumiaji au abiria kwa ajili ya malipo ya huduma zinazodhibitiwa kwa kuzingatia mahitaji yaliyoainishwa katika kanuni hizi.

"mfumo wa tiketi mtandao" maana yake ni mfumo uliojaribiwa na kuidhinishwa na Mamlaka kutoa tiketi mtandao;

"Mfumo Mkuu wa Tiketi Mtandao" maana yake ni mfumo mkuu wa kushughulikia na kudhibiti utoaji wa tiketi mtandao unaojumuisha mfumo wa tiketi za mtandao wa mmiliki, kwa ajili ya kutoa taarifa pamoja na ufuatiliaji wa kumbukumbu unaosimamiwa na Mamlaka;

"mmiliki wa mfumo wa tiketi mtandao" maana yake ni taasisi ya serikali, kampuni au chama cha ushirika ambacho mfumo wake wa tiketi mtandao umeidhinishwa kutumika na Mamlaka;

"mtoa huduma" maana yake ni mtu anayetoa huduma zinazodhibitiwa na aliyeunganishwa na mfumo wa tiketi mtandao ulioidhinishwa na Mamlaka.

## SEHEMU YA PILI
## MAOMBI NA USAJILI WA MFUMO WA TIKETI MTANDAO

Maombi ya kibali cha mfumo wa tiketi mtandao

**4.**-(1) Mtu anayetaka kutoa huduma ya mfumo wa tiketi mtandao anapaswa kuomba kibali kupitia Fomu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza, na kulipia ada ya maombi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Maombi chini ya kanuni ndogo (1) yataambatishwa na nyaraka zifuatazo:

(a) nakala ya cheti cha usajili wa kampuni au chama cha ushirika;
(b) nakala ya leseni ya biashara;
(c) nakala ya hati miliki ya eneo au mkataba wa pango wa ofisi;
(d) cheti cha kulipa kodi;
(e) cheti cha namba ya utambulisho wa mlipa kodi.

Vigezo vya utoaji kibali kwa mfumo wa tiketi mtandao

**5.** Mfumo wa tiketi mtandao unaostahiki kupewa kibali chini ya Kanuni hizi ikiwa utatimiza vigezo vifuatavyo-

(a) uwe unamilikiwa na taasisi ya serikali, chama cha ushirika au kampuni iliyosajiliwa Tanzania;

(b) uwe umeunganishwa na mfumo wa usimamizi wa malipo ya mapato wa kielectroniki;

(c) uwe una uwezo wa kuunganishwa na mifumo ya Mamlaka, Mfumo Mkuu wa Tiketi Mtandao na mfumo wowote kama inavyohitajika;

(d) umeidhinishwa na mamlaka zinazohusika;

(e) uwe wa kitanzania;

(f) uwe na mmiliki mwenye wafanyakazi wenye taaluma husika; na

(g) uwe na ulinzi dhidi ya vamizi za kimtandao.

Kuunganisha na uangalizi wa ulinzi wa mitandao

**6.**-(1) Mamlaka baada ya kupokea maombi, itahakiki utekelezaji wa matakwa ya kanuni ya 5.

(2) Mamlaka baada ya kujiridhisha na kanuni ndogo (1) itamtaka mwombaji kutoa-

(a) timu ya ufundi ya mwombaji ambayo itafanya kazi ya kuunganisha mifumo pamoja na Mamlaka;

(b) nafasi kwa Mamlaka kufanya majaribio ya mwingiliano na kutathmini madhaifu kwenye mfumo;

(c) uthibitisho wa kushughulikia majanga na mpango wa mwendelezo wa huduma.

Maamuzi ya maombi

**7.**-(1) Mamlaka inaweza ndani ya siku kumi na nne baada ya kukamilika kwa ujumuishaji na ukaguzi wa usalama wa mtandao, kuidhinisha mfumo maalumu wa tiketi mtandao na kumsajili muombaji kama mmiliki anayedhibitiwa wa mfumo wa tiketi mtandao.

(2) Mamlaka inaweza kukataa maombi ya mfumo wa tiketi mtandao endapo mwombaji-

(a) atashindwa kukamilisha vigezo chini ya kanuni hii;

(b) atashindwa kuthibitisha umiliki wa mfumo;

(c) anakosa uwezo wa kuendesha mfumo;
(d) anatoa taarifa za mfumo mbazo siyo sahihi;
(e) anajihusisha na vitendo vya uongo;
(f) atashindwa kukamilisha kujiunga na mfumo; na
(g) atashindwa kupita kipimo cha majaribio ya ulinzi wa mtandao.

(3) Endapo Mamlaka itakataa kuidhinisha maombi ya mfumo wa tiketi mtandao itamuagiza mwombaji kurekebisha makosa yaliyotambulika na kuwasilisha tena kwa Mamlaka ndani ya siku kumi na nne kwa ajili ya mapitio.

(4) Endapo mwombaji atashindwa kufanya marekebisho ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kukataliwa kupewa kibali atatakiwa kuleta maombi mapya.

Cheti cha kibali

**8.**-(1) Mamlaka itatoa cheti cha kibali kwa mmiliki wa mfumo wa tiketi mtandao ulioidhinishwa.

(2) Cheti cha kibali kitakuwa halali kwa kipindi cha miaka miwili na kinaweza kuhuishwa.

(3) Mmiliki wa mfumo atatakiwa kulipa ada zilizoainishwa katika Jedwali la Pili la kila baada ya miaka miwili.

Kuhuisha cheti cha kibali

**9.**-(1) Mwenye cheti cha kibali atatakiwa kuwasilisha maombi ya kuhuisha cheti hiko ndani ya siku thelatini kabla ya kuisha kwa muda wa cheti kwa kutumia Fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi ya kuhuisha cheti yataambatishwa pamoja na nyaraka zifuatazo-

(a) nakala ya leseni ya biashara halali;
(b) uthibitisho wa malipo ya tozo za Mamlaka kwa mwaka ulioisha;
(c) cheti halali cha mlipa kodi; na
(d) nakala ya hati ya miliki au mkataba wa pango wa ofisi ikiwa kuna mabadiliko.

(3) Mamlaka inaweza kuhuisha cheti cha kibali chini ya Kanuni hizi baada ya kupokea maombi ya kuhuisha.

Kusimamisha au kufuta cheti cha kibali

**10.**-(1) Mamlaka inaweza kusimamisha au kufuta cheti cha kibali ya mfumo wa tiketi mtandao iwapo kutakuwa na-

(a) uthibitisho wa vitendo vya kutokuwa mwaminifu au uongo kwa mmiliki wa mfumo;

(b) kushindwa kuendesha mfumo;

(c) kushindwa kurekebisha kutokufanya kazi kwa mfumo ndani ya siku saba;

(d) uthibitisho wa uvunjaji wa taarifa za faragha na ulinzi wa taarifa;

(e) uthibitisho wa kuwepo kwa madhaifu katika ulinzi wa mfumo; na,

(f) uvunjifu wa masharti yoyote ya Kanuni hizi na mmiliki wa mfumo wa tiketi mtandao

(2) Endapo mmiliki wa mfumo wa tiketi mtandao atasimamishiwa cheti cha kibali kutokana na sababu zilizo orodheshwa chini ya kanuni ndogo ya kwanza, mmiliki wa mfumo wa tiketi mtandao atahakikisha mtoa huduma anaendelea kupata huduma au taarifa zake zitakazo muwezesha kuendelea kupata huduma kutoka kwa mmiliki mwengine wa tiketi mtandao.

(3) Sababu zakusimamisha au kufuta cheti chini ya kanuni ndogo ya (1) zinaweza kutumika kama sababu za kumuondolea sifa mwombaji kipindi cha kuhuisha cheti cha kibali.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA KUENDESHA MFUMO WA TIKETI MTANDAO

Masharti kwa mmiliki wa mfumo wa tiketi mtandao
T.S Na. 82 la 2020

**11.** Mmiliki wa mfumo wa tiketi mtandao atahitajika-

(a) kumpa ruhusa mtoa huduma kutumia mfumo ulioidhinishwa kutolea tiketi mtandao kwa mtumiaji wa huduma zinazodhibitiwa;

(b) kutunza na kutoa kwa mamlaka kanzidata ya watoa huduma wanaotumia mfumo wake;

(c) kutoa ruhusa kwa Mamlaka kufanya ukaguzi wa mfumo, majaribio ya mwingiliano na tathmini ya madhaifu kwenye mfumo;

(d) kumiliki kituo cha huduma kwa wateja chenye namba za kupiga simu bure;

(e) kuajiri wafanyakazi wenye vigezo wa kuendesha mfumo wa tiketi mtandao;

(f) kutumia viwango na tozo zilizoidhinishwa katika Kanuni za Tozo za Mamlaka;

(g) kuhakikisha kuwa watoa huduma wamesajiliwa kwenye mfumo mkuu wa tiketi mtandao kuendana na wakati uliopo;

(h) kuhakikisha kuwa ratiba zote za mabasi zinapatikana katika mfumo mkuu wa tiketi mtandao kwa wakati;

(i) kuhakikisha kuwa mfumo ulioidhinishwa unakusanya na kutenga tozo za Mamlaka;

(j) kuhakikisha kuwa mfumo unauwezo wa kutengeneza tiketi mtandao kwa njia ya nakala tete nan akala mango;

(k) kuhakikisha kuwa mfumo una uwezo wa kuwasilisha miamala ya nauli kwenye akaunti za benki za watoa huduma kwa wakati halisi;

(l) kuhakikisha kuwa mfumo ulioidhinishwa wa tiketi mtandao unaunganishwa na mfumo wa Mamlaka na mifumo mingine husika kwenye usimamizi wa tiketi mtandao;

(m) kuhakikisha mfumo wa tiketi mtandao unapatikana, unaingilika na ni wa kutegemewa muda wote;

(n) kuweka na kutunza miundombinu ambayo mfumo unaweza kutumika;

(o) kuhakikisha usiri, ulinzi wa taarifa na uzingatiaji wa sheria mahususi za ulinzi wa taarifa;

(p) kusuluhisha na kutoa taarifa za mfumo kuwa na hitilafu ndani ya masaa matatu;

(q) kutoa taarifa kwa mamlaka ndani ya dakika thelathini iwapo mfumo unahitilafu na hatua zinazochukuliwa kushughulikia tatizo;

(r) kutokusimamisha huduma kwa sababu za kutolipa au sababu nyingine za uvunjifu kwa mtoa huduma bila kumpa taarifa mtoa huduma huyo kwa kipindi kisichopungua siku saba; na

(s) kuhakikisha mfumo wa tiketi mtandao una uwezo wa kutoa orodha ya abiria ambayo maudhui yake yatajumuisha jina la abiria, namba ya siti, namba ya simu ya mkononi, tarehe ya safari, namba ya usajili wa chombo cha usafiri na nauli iliyolipwa.

Masharti kwa mtoa huduma

**12.** Mtoa huduma atatakiwa-

(a) kuhakikisha kuwa chombo cha usafiri kimesajiliwa kwenye mfumo wa tiketi mtandao ulioidhinishwa na Mamlaka;

(b) kuhakikisha kuwa ratiba za chombo cha usafiri zimerushwa kwenye mfumo wa tiketi mtandao ulioidhinishwa na Mamlaka ndani ya muda huo;

(c) kutumia mfumo ulioidhinishwa na Mamlaka kwenye kutoa tiketi mtandao;

(d) kuhakikisha kwamba tozo zote zinazotakiwa kwa kutumia mfumo wa tiketi mtandao zinatumwa kwa wakati;

(e) kuwapa wafanyakazi waliopo kwenye chombo cha usafiri kifaa cha kutolea tiketi mtandao;

(f) kutoa taarifa kwa wakati kwa mmiliki wa mfumo wa tiketi mtandao iwapo mfumo una hitilafu;

(g) kutenga tozo za Mamlaka kwa malipo yaliyofanyika kwa fedha taslimu;

(h) kutoa taarifa kwa Mamlaka na kwa mmiliki wa mfumo wa tiketi mtandao endapo chombo cha usafiri hakionekani kwenye mfumo mkuu;

(i) kuhakikisha kuwa kiasi kilichokusanywa ndicho kinachoonekana kwenye tiketi mtandao;

(j) kutoa tiketi moja ya mtandao na orodha ya abiria kwa huduma maalum za kukodisha; na

(k) kutokutumia nembo ya Mamlaka kutangaza biashara yake.

Uteuzi wa wakala

**13.** Mtoa huduma anaweza kuteua wakala wa mfumo wa tiketi mtandao na kutakuwa na makubaliano kati yao kuhusu majukumu yao.

Masharti kwa wakala wa huduma ya tiketi mtandao

**14.** Wakala atatakiwa-

(a) kuhakikisha kuwa kiasi kamili cha nauli kilichotozwa ndicho kinachoonekana kwenye tiketi mtandao;

(b) kutumia mfumo ulioidhinishwa na Mamlaka kutoa tiketi mtandao;

(c) kuhakikisha kuwa tiketi mtandao inayotolewa ina taarifa muhimu za mtumiaji;

(d) kuhakikisha kuwa tozo za Mamlaka zinalipwa kwa wakati halisi;

(e) awe na cheti cha usajili wa mlipa kodi; na

(f) kutokutumia nembo ya Mamlaka kutangaza biashara yake.

## SEHEMU YA NNE
## LUGHA YA MFUMO WA TIKETI MTANDAO NA MAUDHUI YA TIKETI MTANDAO

Lugha ya tiketi mtandao

**15.** Mfumo wa tiketi mtandao utatakiwa kuwa na lugha mbili ya Kiingereza na Kiswahili.

Maudhui ya tiketi mtandao

**16.** Tiketi mtandao itakuwa na taarifa za msingi zifuatazo-

(a) msimbo wa QR na msimbo wa uthibitishaji;

(b) anwani na namba ya simu ya mtoa huduma;

(c) namba ya usajili wa chombo cha usafiri;

(d) tarehe ya kutolewa;

(e) tarehe na muda wa kuondoka, na matarajio ya muda wa kuwasili;

(f) nauli;

(g) njia mahsusi ya safari;

(h) jina la afisa au wakala aliyetoa; na

(i) ikiwa kwa vyombo vya kubeba abiria-

(i) jina kamili na nambari ya simu ya abiria;

(ii) namba ya siti;

(iii) kituo cha kupanda na kushuka; na

(iv) muda wa kuripoti na muda wa kuanza safari.

## SEHEMU YA TANO
## USIMAMIZI WA MFUMO WA TIKETI MTANDAO

Kamati ya

**17.**-(1) Mkurugenzi Mkuu ataunda Kamati ya Wataalamu wa Mfumo wa Tiketi Mtandao ili kusaidia Mamlaka

watalaamu wa mfumo tiketi mtandao

katika masuala ya kiufundi yanayohusu usimamizi wa Kanuni hizi.

(2) Mkurugenzi Mkuu atateua watumishi wasiopungua watano ndani ya Mamlaka ambao watahusika na utungaji na utekelezaji wa masuala yote yanayohusu usimamizi wa Kanuni hizi.

(3) Kamati ya Wataalamu iliyoundwa chini ya kanuni ndogo ya (1) ya Kanuni hii itakuwa na Mwenyekiti na Katibu watakaoteuliwa na Mkurugenzi Mkuu.

(4) Kamati ya Wataalamu itaishauri Mamlaka juu ya masuala yote yanayohusu usimamizi wa Kanuni hizi ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

(a) kumshauri Mkurugenzi Mkuu kuhusu kuidhinishwa au kukataa kuidhinishwa kwa mfumo wa tiketi mtandao baada ya kuridhika au kutoridhika na sifa maalum za kitaalam na kiutendaji;

(b) kukagua mfumo wa tiketi mtandao ulioidhinishwa na kutoa mapendekezo muafaka kwa Mkurugenzi Mkuu; na

(c) kumshauri kufuta leseni ya mmiliki wa mfumo wa tiketi mtandao endapo imethibitishwa kutenda kinyume na Kanuni hizi.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA JUMLA

Takwa la mkataba

**18.** Mtoa huduma anatakiwa kuingia makubaliano na mmiliki wa mfumo wa tiketi mtandao ikitokea mtoa huduma ni tofauti na mmiliki.

Uhamisho wa abiria

**19.** Itakuwa ni wajibu wa mtoa huduma kutoa taarifa kwa Mamlaka husika kuhusu uharibifu utakaopelekea uhamisho wa abiria kwenda kwenye chombo cha usafiri kingine na kusababisha upotevu wa mapato.

Makosa na adhabu

**20.** Mtu atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki tano lakini isiyozidi milioni moja au kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka

miwili au vyote kwa pamoja.

Mapitio T.S Na. 73 la 2020.

**21.** Mtu ambaye hataridhishwa na maamuzi ya Mamlaka chini ya Kanuni hizi anaweza, ndani ya siku kumi na nne kutoka siku ya maamuzi, kuomba kufanya mapitio, kwa mujibu wa Kanuni ya Utaratibu wa Mapitio ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini.

Rufaa Sura ya 285.

**22.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Ushindani, mtu ambaye hataridhishwa na maamuzi ya Bodi anaweza kukata rufaa Baraza la Ushindani.

*Tangazo la Serikali Na.23 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 4(1) na 9(1)*

FOMU YA MAOMBI

1. AINA YA MAOMBI / WEKA ALAMA YA TIKI KATIKA SANDUKU HUSIKA

| | |
|---|---|
| Mpya | |
| Kuhuisha | |
| Kurudufu | |

2. TAARIFA ZA MWOMBAJI WA CHETI

Jina kamili la Mwombaji …………..............................................................

(Jina/Kampuni/Ushirika – kwa HERUFI KUBWA)

Anwani ……………………………………….........

Simu ya Ofisi/Simu ya kiganjani: …………………………………

Simu ya kiganjani ya Mwombaji:...……………………………..…

Barua pepe: ……………………………………..………………

Anwani ya Makazi:

Mtaa: ………………………………….…….

Namba ya Kitalu: ………………………

Namba ya ofisi: ......................................
Namba ya kitalu …………………………

Ushawahi kuwa na maombi yaliyokataliwa, kusimamishwa au kufutiwa
Ndiyo:…..

Hapana:……

Kama ndiyo eleza sababu za kukataliwa, kusimamishwa au kufutiwa maombi
………......................................................................……………………………..

KIAPO/UTHIBITISHO

Mimi ninaapa/ninathibitisha/ Sisi tunaapa/tunathibitisha kuwa taarifa zilizotolewa ni za kweli kwa ufahamu wangu/wetu wote.

Jina Kamili: ……………………………….............    Sahihi: ………………..

Cheo: …………………………………….    Tarehe: ……………...

*Tangazo la Serikali Na.23 (Linaendelea.)*

TAHADHARI:

1. Ijulikane kuwa kutoa taarifa ya uongo ili kupata cheti kilichoidhinishwa ni makosa ambayo yanaweza kuadhibiwa kwa faini au kifungo.
2. Wasilisha taarifa kwa Mamlaka ikitokea mabadiliko yoyote kwenye taarifa zilizopo kwenye fomu hii, kutokufanya hivyo ni makosa chini ya Kanuni hizi.

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

NAMBA YA JALADA LA MMILIKI

………..................................................................

Uhakiki na Kibali

(a) Kibali hakijaidhinishwa:

Weka sababu
…………………………………………………………………………

(b) Kibali kimeidhinishwa:

Tarehe ya kuanza: ……………………..

Tarehe ya kuisha: ……………………......

Jina kamili la Afisa: ………………………………………………………………..

Cheo: ………………………………

Sahihi:………………………………
Tarehe: ………………………………

Kiasi kilicholipwa: ……………….. Namba ya stakabadhi. ………………..
Tarehe:...………………………… Sahihi: ……………………

ANGALIZO: VIAMBATISHO

1. Maombi ya kwanza yataambatishwa na vifuatavyo:
   (a) nakala ya cheti cha usajili wa kampuni au chama cha ushirika;
   (b) nakala ya leseni ya biashara;
   (c) nakala ya hati miliki ya eneo au mkataba wa pango wa ofisi; na
   (d) nakala ya cheti cha mlipa kodi.

2. Kuhuisha:
   (a) uthibitisho wa malipo ya tozo ya Mamlaka kwa mwaka ulioisha;
   (b) nakala ya leseni ya biashara;
   (c) nakala ya cheti cha mlipa kodi; na
   (d) nakala ya hati miliki ya eneo au mkataba wa pango wa ofisi kama kuna mabadiliko.

*Tangazo la Serikali Na.23 (Linaendelea.)*

______________

JEDWALI LA PILI

______________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1) na 8(3))*

ADA

| Na. | Aina | Tsh |
|---|---|---|
| | Ada ya Maombi | 50,000 |
| | Ada ya Cheti cha Kibali | 5,000,000 |

Dodoma,
15 Disemba, 2023

MAKAME MNYAA MBARAWA,
*Waziri wa Uchukuzi*